

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
15 Desemba 2007**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Dominata Rwechungura
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Sudi Saidi Ramadhan

Siku ya uamsho wa mabadaliko ya majira

Tuliongea kuhusu msafara wa baisikeli ya siku ya uamsho wa mabadaliko ya majira iliyotokea jumamosi iliyopita. Watu wa UWABA, JEMA na TCSD walishirikiana kwenye msafara na tulibeba barua zilizosainiwa na mashirika kumi. Tuliendesha baisikeli kutoka Mabibo mpaka ofisi ya Makamu Rais. Kwenye ofisi ya Makamu Rais tulikaribishwa, na Mejah alitoa hotuba kuhusu mabadaliko ya majira na naibu mkuu wa mazingira alijibu na hotuba yake ya kuunga mkono nasi. Baada ya hiyo tulijiandaa kwenda ubalozi wa Merekani lakini tulisimamishwa na polisi ambao walituambia kwamba hatutaruhusu kwenda maeneo ya ubalozi wa Merekani bila barua ya kutualika, na walitupa barua iliyosema hivi. Waandishi wa habari wa Channel 10, gazeti ya Majira na BBC redio walikuwepo, ambao walipata taarifa kuhusu tukio kutoka Dominata.

Wanachama walisema kwamba si sheria kwa polisi kusimamisha msafara kwa sababu tulitoa taarifa kwa polisi na ubalozi wa Merekani kabla ya tukio (Ubalozzi wa Merekani walikataa kutupokea basi tulikuwa tuliamua kwenda pale kama kundi kuacha barua zetu tu). Tuliamua kupata ushauri wa kisheria kutoka shirika la sheria kuhusu haki zetu za sheria na kama polisi wana uwezo kufanya hivi chini ya sheria.

Hata kwenye mazungumzo jiji la Bali, Indonesia serekali ya Merekani wanaziba mazungumzo na maendeleo kwenye swala hili. Wakati wa wiki Elaine aliandika na Juma alipeleka barua kumi kutoka mashirika waliosaini ambazo tulikusudia kuzipeleka siku yenyewe kama kundi, pamoja na barua nyingine ya kusema kusimamisha msafara wetu siyo nzuri kwa demokrasia, mashirika ya siyo ya kiserekali au haki za binadamu hapa Tanzania.

Sosthenes alitoa nakala mbili ya video ya tukio na Ally Saidi Mohammad alisema tunaweza kuiangalia wiki ijayo kwenye TV yake na vidoe player ya rafiki yake.

Elaine alipendekeza kwamba kampeni za mwaka ujao kuhusu swala hili ziendeshe zaidi ya mashirika kama TCSD na UWABA tunaweza kushirikiana nao, kwa sababu TCSD ina maswala haya kwenye katiba yake. Lakini UWABA tumechangia kwenye debate ya swala hili hapa Tanzania.

Guta

Spea za guta zimefika sasa kwenye kampuni ya guta. Tulikubali kwamba Juma na Elaine wachukue hela ya Tsh 55,000 kutoka benki jumatatu na hii pamoja na Tsh 45,000 ambayo Juma bado anayo ya hela ya UWABA itumikwe kwa kununua mipira mpya. Juma na Jumanne watakutana Mabibo saa nne asubuhi jumatatu asubuhi na wataenda kununua pamoja.

Mambo ya hela

Mchango wa Bike Nouveau Fabrique Italy umeingia akaunti ya benki ya UWABA. Tulikubali kupata kadi ya thank you na wanachama watasaini na kuandika jumbe za kuwashukuru.

Wakati wa wiki Elaine na Juma walichukua hela kutoka akaunti ya UWABA wa kurudisha hela ya msafara na T-shirts ambazo Elaine na Mejah walitumia kutoka hela zao binafsi.

Ubalozi wa Uholonzi wametupa hundi ya Tsh 265,000. Inaonekana kuna kosa kwa sababu tulielewa kwamba tutapata Tsh 50,000 zaidi. Elaine atafuatalia wiki hii.

Hela nyingine tutahifadhi kwa ajili ya kodi ya ofisi na gharama za tukio, lakini tulikubali kutumia hela kama Tsh 200,000 kwa kununua helmeti za mitumba na kutengeneza T-shirts kwa ajili ya wanachama ambao wanahudhuria sana mikutano.

Ofisi

Bao moja mpya ipo juu na bao zingine bado zinatengenezwa - Ally Saidi Mohammed atamaliza wiki hii.

Elaine bado hajafanya kazi ya kuprintia dondoo za Kiswahili.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji

Bwana Wemba bado hajajibu barua yetu ya kuomba semina ya usalama barabarani. Elaine alijaribu kumpigia simu lakini hapatikani. Atafuatalia tena wiki hii.

Halmashauri ya Jiji na TANROADS

Ally Saidi Mohammed alisema ataleta photocopy za michoro ya Barabara ya Morogoro wiki ijayo. Bado hatujapata majibu ya barua zetu kutoka halmashauri ya jiji wala TANROADS.

Nyinginezo

Wamba memorial fund bado hawajatumia uamuzi wao kuhusu mradi wa usalama barabarani.